**Tangazo kwa Umma**

**KULINGANA NA KANUNI YA PILI YA KANUNI ZA SHERIA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (UNUNUZI MKUBWA, UCHUKUAJI NA UUNGANISHAJI) ZA MWAKA 2006 (KANUNI)**

**SCANCEM INTERNATIONAL DA**
(Imesajiliwa nchini Norway)
(Namba ya Usajili 943 513 716)
("**Scancem**")

---

**TAARIFA KWA WANAHISA WA TANGA CEMENT PLC ILIYOIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA ("CMSA")**

---

Scancem International DA (**Scancem au Mtoa Ofa**) inatoa ofa kwa wanahisa wa Tanga Cement PLC (**Tanga Cement au Kampuni-Lengwa**) ambapo inanuia kununua kwa ujumla hisa za Tanga Cement (**hisa za Tanga**), tofauti na zile ambazo tayari inazimiliki au kuzidhibiti, kwa mujibu wa Kanuni ya pili ya Kanuni za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (Ununuzi Mkubwa, Uchukuaji na Uunganishaji ) za mwaka 2006 (Kanuni).

Kwa kufuata Kanuni ya 12(2) ya Kanuni, Bodi ya Wakurugenzi wa Tanga Cement imewasilisha maoni ya haki (fairness opinion) na mapendekezo kwa wanahisa pamoja na Nyaraka ya Ofa (Offer Document) kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

**Taarifa muhimu:**

1. **Mtoa Ofa**: Scancem International DA, kampuni-ubia yenye namba ya usajili 943 513 716 iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria za Norway.
2. **Kiasi**: Mtoa Ofa anataka kununua kiasi cha 6.67% ya hisa za Tanga ambazo Mtoaji hazimiliki au kuzidhibiti kwa sasa; na ambazo jumla yake ni hisa za Tanga 4,248,881 ambapo kila hisa inakadiriwa kuwa Shilingi 20.00 za Tanzania **(TZS 20.00)** kwa kila moja.
3. **Bei/Malipo**: TZS 2,273 kwa kila hisa ya Tanga.
4. **Njia ya Malipo**: Fedha taslimu.
5. **Mtaji wa hisa za Tanga Cement**: Thamani ya hisa zilizotolewa na kulipiwa tayari ni TZS 1,273,420,900, zikijumuisha jumla ya hisa za kawaida 63,671,045 kwa thamani ya TZS 20 kwa kila hisa.
6. **Kiasi cha hisa za Tanga zinazomilikiwa na Scancem kwa sasa**: Scancem kwa sasa inamiliki 68.33% ya hisa zote za Tanga Cement.
7. **Sifa Muhimu za Ofa**: Vipengele na masharti muhimu ya Ofa yameanishwa kama ifuatavyo:
   a) Scancem kupitia Ofa ya Ununuzi wa Jumla iliyopo ndani nyaraka ya Ofa inanuia kununua hisa 4,248,881 za Tanga Cement kutoka kwa mwanahisa yeyote anayeridhia kuziuza kwa Scancem. Endapo wanahisa wataridhia kwa maandishi kuziuza hisa zao kwa Scancem, kwa mujibu wa maelekezo yaliyomo kwenye Nyaraka ya Ofa, Scancem itakuwa na udhibiti wa 75% wa hisa za Tanga (**Ukomo wa Umiliki**). Kiwango hiki cha umiliki/udhibiti kinahusisha hisa ambazo Scancem yenyewe inazimiliki kwa sasa pamoja na hisa zinazomilikiwa na kampuni zake tanzu. Mwanahisa atakayeridhia kwa barua kuuza hisa zake (Barua ya Kuridhia) hataruhusiwa kubatilisha uamuzi wake baada ya kupokelewa kwa Barua ya Kuridhia (Acceptance Letter).

b) Ukomo wa Umiliki unaweza kupandishwa endapo Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) itaruhusu hivyo kabla ya kutangazwa kwa matokeo ya walioridhia kuuza hisa zao.

c) Endapo mwitikio wa wanahisa utakuwa mkubwa kiasi kwamba hisa zitakazotolewa kwenye zabuni zitakuwa nyingi kuzidi hisa zinazotakiwa kufikia Ukomo wa Umiliki, Scancem itanunua hisa kwa uwiano (pro-rata) ili kuepuka kuvuka Ukomo wa Umiliki.

Wanahisa wawasiliane na Wakala yeyote aliyesajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Mshauri wa Uwekezaji aliyesajiliwa au Scancem kwa ajili kupatiwa Nyaraka ya Ofa na maelekezo ya kina kuhusu mchakato mzima unaohusiana na Ofa hii.

8. **Malipo:** Scancem inatoa ofa ya kulipa TZS 2,273 kwa kila hisa ya Tanga.

9. **Vyanzo vya fedha**: Scancem imeshathibitisha upatikanaji wa fedha yote inayohitajika kununua hisa za Ofa kutoka vyanzo mbalimbali vya nje na vya ndani.

10. **Malengo na Kusudi la Ofa hii:** Kuhakikisha kuwa Tanga Cement inaendelea kuwa kampuni bora inayoendeshwa kwa faida na yenye uwezo wa kuzalisha saruji zaidi ili kuwezesha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kupitia ujenzi wa miundombinu, ustawi wa biashara na ujenzi wa miradi ya watu binafsi. Heidelberg Materials AG, ambayo ni kampuni-mama ya Scancem ("**Heidelberg Materials**"), imekuwepo nchini Tanzania, kupitia kampuni yake tanzu ya Tanzania Portland Cement Public Limited Company (Twiga Cement), tangu mwaka 1966. Heidelberg Materials ina mpango wa kuendelea kuleta uzoefu wake wa nje kwa kutoa utaalam kama kampuni kinara inayozalisha saruji na kuendesha shughuli zake kwa weledi zaidi nchini Tanzania.

11. **Ratiba**: Ofa hii itatekelezwa mara tu Masharti yote yatakapokamilika (ikiwa inafaa). Hili litafanyika haraka iwezekanavyo mara baada ya kuchapishwa kwa Tangazo hili.

a) Tarehe ya kubainisha wanahisa watakaopewa Nyaraka ya Ofa itakuwa ni siku ambayo Tangazo hili litachapishwa 1 Julai 2025.

b) Tarehe za kuanza na kusita kupokea zabuni (Barua za Kuridhia-Acceptance Letters) ni:

   a. Kuanza: 1 Julai 2025; na

   b. Kufunga: 22 Julai 2025, au tarehe nyingine itatakayoamuliwa na Scancem.

c) Utaratibu ambao wanahisa wataufuata kuridhia kuuza hisa zao kwa Scancem umeelezwa kwa kina kwenye Nyaraka ya Ofa.

d) Tarehe ambayo malipo kwa wanahisa watakaouza hisa zao kwa Scancem kupitia hii Ofa yatafanyika imeelekezwa katika Kanuni.

12. **Idhini za kisheria**:

a) Hakuna idhini za kisheria zinazohitajika kwa sasa kuhusiana na Ofa hii.

***Kuhusu Tanga Cement***

*Tanga Cement ilisajiliwa nchini Tanzania mwaka 1980 kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ikiwa kampuni ya umma yenye dhima ya ukomo. Kampuni hiyo iko takribani kilomita 15 kutoka katikati ya Jiji la Tanga. Tanga Cement ina kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha klinka na saruji kwa kutumia chokaa inayopatikana katika eneo la kiwanda.*

***Kuhusu Scancem***

*Scancem ni kampuni-ubia iliyoanzishwa huko Norway katika mji wa Oslo mwaka 1986. Namba yake ya usajili ni 943 513 716 na anuani yake iliyosajiliwa ni: c/o Heidelberg Materials Norway AS, Lilleakerveien 2A, 0283 Oslo, Norway. Wabia wake ni kampuni mbili zilizosajiliwa Norway, kampuni zote mbili zinamilikiwa kwa asilimia 100 na Heidelberg Materials. Scancem ni sehemu ya wauzaji wakubwa wa vifaa vya mbao na vifaa vingine vya ujenzi na inazalisha, inauza na kusambaza simenti.*